# TUJIFUNZE BIBLIA

## *SOMO LA 5*

### UMOJA WA KANISA LA KRISTO

Watu wa siku zetu wamejigawa katika makanisa mengi ya kimadhehebu, wakidhani kwamba ndivyo alivyotaka Mungu. Jel madhehebu yametoka kwa Mungu? Ebu! tuone maneno ya Yesu.

### YESU ALIJENGA KANISA MOJA TU

Kabla Yesu hajafa, alitoa ahadi kwa wanafunzi wake akisema "*nitalijenga kanisa langu*" (Mathayo 16:18). Tazama! Yesu hakusema makanisa au madhehebu kana kwamba ni mengi bali alisema kanisa lake likiwa ni moja.

1. Je! katika Mathayo 16:18, Yesu alisema atayajenga makanisa mengi au kanisa moja tu? ____________________

Yesu alifananisha kanisa lake na kundi la kondoo akisema:

"*Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja.*" Yohana 10:16

2. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba inatakiwa kwa kondoo (yaani Wakristo) wote wawe makundi mangapi? ____________________

Yesu hakutaka fitina na faraka ya kimadhehebu. La! bali aliwaombea wanafunzi wake akisema:

"*Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.*" Yohana 17:20-21

3. Yesu aliwaombea Wakristo wote wawe na nini? ____________________
4. Wakristo wote wakiwa na umoja, ulimwengu utapata kusadiki kwamba Yesu alitumwa na nani? ____________________

Wapagani wengi wanakosa kuingia katika kanisa kwa sababu ya faraka ya kimadhehebu ya siku zetu. Wanashangaa kuona jinsi kila dhehebu linavyofundisha mambo tofauti na dhehebu jingine. Kisha, wanakata tamaa wakidhani kwamba dini ya kikristo ni upuuzi tu. Ndiyo maana Yesu alitaka tuwe na umoja. Tena tumeamriwa:

"*… kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. <u>Mwili mmoja</u>, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, <u>imani moja</u>, ubatizo mmoja.*"

Waefeso 4:3-5

5. Imewapasa Wakristo kujitahidi kuuhifadhi nini? ____________________

6. Je! umoja utaleta fitina au utaleta Amani? ____________________

7. Yesu ana miili mingapi? ____________________

8. Kuna imani za aina ngapi zinazokubaliwa na Mungu? ____________________

Katika mistari hii ya Waefeso tumejifunza kwamba Yesu ana mwili mmoja tu. Je! mwili huo ni kitu gani? Mwili huo ni kanisa lake Kristo. Twasoma:

*"*(Mungu) *akavitia vitu vyote chini ya miguu yake* (Yesu), *akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"

Waefeso 1:22-23

"*Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru.*" 1Wakorintho 12:13

9. Je! mwili ule mmoja wa Yesu ni nini? ____________________

10. Ikiwa mwili ni kanisa na ikiwa kuna mwili mmoja tu, basi kuna makanisa mangapi?

____________________

## MADHEHEBU NA MAJINA YAO

Madhehebu maana yake nini? Katika kitabu cha Kamusi ya Kiswahili tunaambịwa kwamba madhehebu maana yake ni "jamii ya watu wafuatao dini ya namna moja wakifuata mafundisho tofauti na madhehebu mengine." Kwa mfano, Wayahudi wa zamani walianza kuchanganya mapokeo ya watu pamoja na maneno ya Mungu. Basi, palitokea utengano kati yao wakijigawa katika madhehebu mawili tofauti, yaani Mafarisayo na Masadukayo (Matendo 23:6-8). Kati ya madhehebu haya, waliokuwa wakifuata ukweli wa neno la Mungu walikuwa Mafarisayo (Matendo 26:5). Kwa hiyo, Mungu hakufurahi kuona madhehebu mbalimbali; maana panapo madhehebu lazima wengine wao wamepotea. Ndiyo maana hakuna umoja kati ya madhehebu. Basi, hata siku zetu. Mungu hataki fitina ya kimadhehebu. Ndiyo maana Paulo aliwaonya Wakristo wa mji wa Korintho akisema:

"*Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja. Kwa maana, ndugu zangu, nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. Basi, maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu husema, Mimi ni wa Paulo, na, Mimi ni wa Apolo, na, Mimi ni wa Kefa, na, Mimi ni wa Kristo. Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! mlibatizwa kwa jina la Paulo?... Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu? Maana hapo mtu mmoja asemapo, Mimi ni wa Paulo; na mwingine, Mimi ni wa Apolo, je! ninyi si wanadamu?... Basi ndugu, mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu, ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa; ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe… Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu.*" 1Wakorintho 1:10-13; 3:3-4; 4:6; 14:33

11. Paulo aliwasihi Wakristo kwa jina la Bwana kwamba wote wanene nini?

____________________

12. Je! madhehebu yanena mamoja? ____________________

13. Je! Wakristo wanapojitenga katika madhehebu wanaleta fitina au wanaleta amani?

____________________

14. Je! inaruhusiwa kwa Wakristo kujiita kwa majina ya wanadamu? ____________________

15. Je! Wakristo wameruhusiwa kupita yale yaliyoandikwa katika Biblia? ____________________

16. Je! machafuko (au faraka) ya kimadhehebu yametoka kwa Mungu? ____________________

Tena, Paulo aliwasihi Wakristo wa mji wa Filipi; akisema:

"*Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, ili, nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo, niyasikie mambo yenu, kama mnasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili.*" Wafilipi 1:27

17. Imewapasa Wakristo kusimama imara kwa moyo mmoja wakishindania nini?

____________________

**MWANZO WA KANISA LA KRISTO**

Tumesoma maneno ya Yesu akasema "nitalijenga kanisa langu" (Mathayo 16:18). Kanisa la Kristo si jengo bali ni watu waliookolewa kutoka dhambini. Katika Matendo 2:47 twasoma "*Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*" Basi, Biblia inafundisha kwamba mwanzo wa kanisa la Kristo ulikuwa katika mji wa Yerusalemu katika siku ya Pentekoste. Maana, siku ile watu 3,000 waliokolewa wawe kanisa (Matendo 2:1-47). Kwa hiyo, karibu miaka 2,000 imepita tangu Kristo alipoanzisha kanisa lake (kanisa lilianzishwa mnamo mwaka 33 B.K.)

18. Kanisa la Kristo si jengo bali ni watu waliofanya nini? ____________________

19. Karibu miaka mingapi imepita tangu Yesu alipoanzisha kanisa lake? ____________________

Ingawa kanisa lilianzishwa huko Yerusalemu, walakini lilienea sana kabla mitume hawajafa. Kwa mfano twasoma:

"*Siku ile kukatukia adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu; wote wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria, isipokuwa hao mitume… Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno. Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo… Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake.*" Matendo 8:1,4-5,12

Wakristo hawa wa Samaria hawakuwa dhehebu la kanisa la Yerusalemu. La! bali walihesabiwa kuwa viungo vya mwili ule mmoja wa Kristo, yaani, kanisa lake (1Wakorintho 12:13; Matendo 2:47). Vivyo hivyo, katika Biblia twasoma habari ya makanisa mengine ya Kristo. Kwa mfano, Wakristo walioishi katika mji wa Efeso waliitwa kanisa la Kristo la mji ule. Hali kadhalika, twasikia habari ya makanisa yaliyokuwapo Korintho, Ikonio, Rumi, Kolosai, Filipi, na mahali pengine. Kama tulivyosema, makanisa hayo hayakuwa madhehebu. La! bali makanisa hayo yote yalikuwa ya namna moja na imani moja yakiongozwa na neno la Kristo. Kumbuka, "*Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa Amani*" (1Wakorintho 14:33). Basi, ndiyo maana Paulo aliandika barua kwa Wakristo wa mji wa Rumi akasema "*Makanisa yote ya Kristo yawasalimu*" (Warumi 16:16).

20. Je! makanisa yaliyokuwapo Korintho, Ikonio, Rumi na mahali pengine yalikuwa madhehebu ya kanisa la Yerusalemu? ____________________

**KANISA HALIKUJENGWA JUU YA PETRO**

Baadhi ya watu wameelewa vibaya maneno ya Yesu aliposema "*nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu*" (Mathayo 16:18). Kwa sababu jina Petro tafsiri yake ni jiwe (Yohana 1:42) basi watu wengi hudhani kwamba kanisa limejengwa juu ya Petro. Walakini, Yesu hakusema kwamba atalijenga kanisa juu ya <u>jiwe</u> (Petro) bali juu ya <u>mwamba</u>. Kuna tofauti kubwa kati ya jiwe na mwanba. Petro hajawahi kuitwa mwamba katika Biblia. La! bali <u>Petro mwenyewe alimwita Yesu kuwa mwamba.</u> Petro alisema:

"*Mmwendee yeye* (Yesu)*, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima… Basi, heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini. Bali kwao wasioamini, jiwe walilolikataa waashi, limekuwa jiwe kuu la pembeni. Tena, jiwe la kujikwaza mguu, na mwamba wa kuangusha. Kwa maana hujikwaza kwa neno lile, wasiliamini, nao waliwekwa kusudi wapate hayo.*" 1 Petro 2:4,7-8

21. Petrro alisema kwamba jiwe kuu la pembeni na mwamba wa kuangusha alikuwa nani?

____________________

Paulo alisema: "*Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye <u>Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni</u>. Katika yeye jengo lote lina ungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana.*" Waefeso 2:20-21

"*Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu. Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. <u>Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uiokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo.</u>*" 1 Wakorintho 3:9-11

22. Jiwe kuu la pembeni ni nani? ____________________

23. Mtume Paulo hakusema kwamba msingi pekee wa kanisa ulikuwa Petro, bali msingi wa kanisa ulikuwa nani? ____________________

**MKUU WA KANISA**

Kabla Yesu hajapaa mbinguni aliwaambia wanafunzi wake: "*Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani*" (Mathayo 16:18). Baadhi ya watu leo hudhani kwamba Yesu alipopaa alimwachia Petro mamlaka awe mkuu katika kanisa. Watu hawa hutukumbusha maneno ya Yesu alipomwambia Petro "*lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni*" (Mathayo 16:19). Walakini, Yesu alitoa ahadi ile ile kwa mitume wote wengine pia akiwaeleza:

"*Amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.*" Mathayo 18:18

Neno lile "mtakayoyafunga" huonyesha waziwazi jinsi Yesu alivyotoa ahadi hii kwa watu wengi wala si kwa Petro tu.

24. Yesu alipomwambia Petro "lo lote utakalolifunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni" je! alikuwa akimpa Petro uwezo kuliko mitume wengine? ____________________

Watu wengine husema kwamba Yesu alimfanya Petro kuwa mkuu wa kanisa alipomwambia "chunga kondoo zangu" (Yohana 21:16). Walakini, maneno haya ya Yesu hayakumfanya Petro awe mkuu. La! bali Yesu alikuwa akionyesha kwamba Petro atashiriki kazi ya uchungaji pamoja na wazee wengine wa kanisa. (Kazi ya wazee wa kanisa nị kuchunga na kulisha Kanisa _ soma Matendo 20:17,28). Basi, ndiyo maana Petro mwenyewe alisema:

"*Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia… Na Mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka.*" 1 Petro 5:1-2,4

25. Je! Petro alikuwa mchungaji mkuu wa kanisa? ____________________

Wakristo wa mji wa Yerusalemu waliwaheshimu sana Yakobo, Yohana, na Kefa (Petro). Walakini, Paulo alisema:

"*Lakini wale wenye sifa ya kuwa wana cheo; (walivyokuwa vyo vyote ni mamoja kwangu; Mungu hapokei uso wa mwanadamu); nasema, hao wenye sifa hawakuniongezea kitu… (maana yeye aliye mwezesha Petro kuwa mtume wa waliotahiriwa ndiye aliyeniwezesha mimi kwenda kwa Mataifa); tena walipokwisha kuijua ile neema niliyopewa; Yakobo, na Kefa, na Yohana, wenye sifa kuwa ni nguzo, walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika; ili sisi tuende kwa Mataifa, na wao waende kwa watu wa tohara… Lakini Kefa alipokuja Antiokia, nalishindana naye uso kwa uso, kwa sababu alistahili hukumu, Kwa maana kabla hawajaja watu kadha wa kadha waliotoka kwa Yakobo, alikuwa akila pamoja na watu wa Mataifa, lakini walipokuja wao, akarudi nyuma akajitenga, huku akiwaogopa walio tahiriwa.*" Wagalatia 2:6,8-9,11-12

26. Je! Paulo alikubali kwamba Yakobo, Yohana na Kefa (Petro) walikuwa wenye cheo mbele ya Mungu? ____________________

27. Je! mitume hao waliweza kumwongezea Paulo kitu? ____________________

28. Paulo alishindana na Petro (Kefa) huko Antiokia kwa sababu Petro alistahili nini? ____________________

Watu wengine husema kwamba Petro alikuwa Papa (yaani, baba) wa kanisa. Jambo hili si kweli maana Yesu mwenyewe alisema:

"*… msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo.*" Mathayo 23:9-10

29. Tafsiri ya majina "Papa" na "Padiri" ni "baba". Je! Yesu alitaka Wakristo waitwe baba katika kanisa lake?

30. Yesu alisema kwamba Wakristo watakuwa na viongozi wangapi?

31. Kiongozi wa Wakristo ni nani?

Basi, Yesu hakumwachia mwanadamu ye yote mamlaka awe mkuu wa kanisa. La! Hata ingawa Yesu yuko mbinguni, lakini yeye peke yake ni kichwa (yaani, kiongozi) cha kanisa. Twasoma:

"(Mungu) *aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*" Waefeso 1:20-23

32. Mungu amemweka nani awe juu sana kuliko ufalme wote na mamlaka, na nguvu, na usultani? ____________________

33. Mungu amemweka nani awe kichwa cha kanisa tangu Yesu alipopaa mbinguni? ____________________

## MAKAO MAKUU YA KANISA

Makao makuu maana yake ni mahali anapoishi mtu mwenye mamlaka, Kwa mfano, Nairobi ni makao makuu ya nchi ya Kenya, maana ndipo anapoishi rais wa Kenya. Je! makao makuu ya Kanisa la Kristo yako wapi? Huko juu tumethibitisha kwamba ni Yesu aliye na mamlaka yote katika kanisa lake. Yesu mwenyewe alisema *"… nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani*" (Mathayo 28:18). Kwa hiyo, alisema "*msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo*" (Mathayo 23:8). Kisha aliwaambia wanafunzi wake "*Nyumbani mwa Baba yangu mna makao nengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi, mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo*" (Yohana 14:2-3). Kumbe! makao makuu ya kanisa la Kristo hayapo hapa duniani bali yako mbinguni ambako aliko Yesu.

34. Mtu mkuu mwenye mamlaka yote katika kanisa ni nani? ____________________

35. Makao makuu ya kanisa la Kristo yako wapi? ____________________

**KUMBUKUMBU LA SOMO HILI**

Katika somo hili tumejifunza kwamba madhehebu hayakutoka kwa Mungu. Yesu alisema atalijenga kanisa moja tu na aliwaombea Wakristo wote wawe na umoja.

Kanisa la Kristo lilianzishwa na Yesu mnamo mwaka 33 B.K. katika mji wa Yerusalemu. Kisha, kanisa likaenea katika miji mingine mingi. Wakristo hawa wa miji mbalimbali waliitwa "makanisa ya Kristo" (Warumi 16:16). Makanisa haya hayakuwa madhehebu, maana yote yalikuwa yakifundisha mamoja. Baadaye, faraka ilitokea katika kanisa la mji wa Korintho kwa sababu Wakristo walianza kujiita kwa majina ya kibinadamu. Paulo aliwakemea sana akiwasihi wote wanene mamoja. Madhehebu hayaneni mamoja, na kwa hiyo, hayatoki kwa Mungu. "Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani" (1 Wakorintho 14:33).

Kanisa halikujengwa juu ya Petro, wala Yesu hakumwachia Petro mamlaka awe mkuu wa kanisa. Yesu peke yake ni mkuu wa kanisa hata leo. Kwa hiyo, makao makuu ya kanisa hayako duniani bali yako mbinguni aliko Yesu.

Basi, mwanafunzi anaombwa awafundishe wenzake somo hili kusudi watu waache faraka na ugomvi wa kimadhehebu. Kumbuka, dini yetu itakuwa bure tukichanganya mapokeo ya wanadamu na maneno ya Mungu (Mathayo 15:3,8-9; Ufunuo 22:18-19).

************************************************************************************

Jina lako …………………………………………………<br>
Anwani yako ……………………………………………

***KANISA la KRISTO***<br>
***Tanzania***